**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
OFISI YA RAIS-TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA ROMBO
**SHULE YA SEKONDARI HOROMBO**
S.L.P 186, MKUU-ROMBO

25/04/2024

**NAMBA ZA SIMU**
MKUU WA SHULE: **+255 784347795 / + 255 652190906,**
MAKAMU MKUU WA SHULE:**+255 782921188/+255 756455756.**
E-MAIL: ____________________________________

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi……………………………
…………………………………………………………
S.L.P……………………………………………………

…………………………………………………………..

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI HOROMBO MWAKA 2024/2025**

## 1.0 UTANGULIZI.

Ninayo furaha kukujulisha kwamba mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule ya Sekondari Horombo iliyopo wilaya ya Rombo Mkoani Kilimanjaro; Tahasusi ya **CBG/HKL**

Shule ipo kilometa 5 toka kituo cha mabasi Mkuu Wilayani. Ni imani yangu kuwa ufikapo shuleni utatumia vizuri nafasi hii uliyotunukiwa na Taifa lako kusoma kwa bidii na maarifa ili kujiletea maendeleo yako binafsi, kwa familia yako na Taifa kwa ujumla.Hivyo unapokuja shuleni lengo lako liwe ni kujifunza kwa bidii ili kupata elimu bora na endelevu.

Aidha, tunaamini kuwa ili ufanikiwe kimasomo lazima uwe na nidhamu ya hali ya juu. Sheria na kanuni za shule nimekufungashia. Soma kwa makini na ujue kuwa ***kumcha Mungu ni chanzo cha maarifa***.

### 1.1. USAFIRI WA KUFIKA SHULENI

Mwanafunzi akifika Moshi mjini kituo kikuu cha mabasi akitokea popote pale, aulize na kupanda magari yaendayo Rombo kupitia Mwika hadi Mkuu Rombo. Nauli ya kutoka Moshi mjini hadi Mkuu Rombo ni Tshs. 4000/= tu. Kwa wanafunzi wanaotoka Dar es Salaam au kupitia Dar es Salaam wapande magari ya *Dar express*, *Tilisho*, *Esther luxury, King Meridian;* yanayokuja moja kwa moja Rombo. Kwa wanaotoka Dodoma wapande *Shabiby, Extra coach* na wanaotoka Singida wapande *Ngasere luxury.* Kwa wanaotoka Mwanza na maeneo mengine ya kanda ya ziwa wapande mabasi yanayofika hadi Moshi mjini na kisha kupanda magari yanayoenda Mkuu – Rombo..

Ukifika stendi ya Mkuu - Rombo wilayani chukua usafiri wa pikipiki (bodaboda) gharama ni Tsh 3000/= tu. Mwambie akupeleke Horombo sekondari utafika salama.

Muhula wa masomo utaanza tarehe**……………….** Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe………………mwisho wa kuripoti ni tarehe…………….. (Kulingana na maelekezo yatakayotolewa na TAMISEMI

## 2. Mambo Muhimu ya Kuzingatia

### 2.1 SARE YA SHULE:

Kila mwanafunzi anatakiwa kuja na sare ya shule iliyoshonwa vizuri kwa maadili ya mwanafunzi awapo shuleni. **Ni marufuku kwa mwanafunzi kuja na nguo fupi na zinazobana, atakayekuja nazo hatapokelewa.**

- Sketi mbili (02) rangi **ya Orange** inayozidi magoti kwa urefu unaokaribia kwenye viatu mshono **–** “**Rinder box**” **mbele na nyuma pembeni marinda madogo matatu.**.
- Mashati mawili (2) meupe ya mikono mirefu yasiyo bana mwili na yenye vishikizo vya kawaida..
- Tai ndefu rangi ya Orange iisiyokuwa na Michirizi
- Soksi nyeupe ndefu jozi 2 au zaidi na viatu vyeusi vya kamba visivyokuwa na visigino virefu, jozi mbili.
- Sweta za shule mbili zenye rangi sawa na sketi (Orange)
- Nguo za michezo jozi moja rangi ya kijani,raba za michezo jozi moja rangi yoyote na truck suit rangi ya dark blue
- Gauni la kushindia (Shamba dress) la rangi ya **dark blue draft ndogo (kunguru)** mshono wa solo, urefu usiopungua inchi 15 kutoka gotini kwenda chini,

- **Mwanafunzi aje na tochi/ taa ya solar na mwamvuli kwa ajili ya kujikinga na mvua**

➢ Kwa wanafunzi Waislamu wanaruhusiwa kuvaa HIJABU nyeupe na sketi ya rangi ya orange.

➢ Mwanafunzi aje na **sweta mbili za kuvaa usiku wakati wa masomo ya usiku rangi nyeusi na zisiwe na maandishi wala alama nyingine yoyote.**

➢ **Mwanafunzi anapaswa kuwa na T-shirt yenye rangi ya dark blue kwa ajili ya EK na Clubs and Hobbies. Mzazi anaweza kumnunulia mtoto wake popote, aidha t-shirt pia zinapatikana kwenye duka la Shula Kwa bei ya sh 11,000.**

***N.B; Mwanafunzi haruhusiwi kuja na nguo nyingine tofauti na sare tajwa.***

### 2.2 MAHITAJI YA DARASANI

Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa na vifaa vya darasani kama ifuatavyo:-

- Madaftari makubwa(Counter Books Q3/Q4) yasiyopungua nane (8), kalamu, rula, penseli, mathematical set, Scientific calculator(Non programmable), file kwa kila somo (kwa masomo ya msingi- principle subjects) kwa ajili ya kutunza mitihani na majaribio.
- Madaftari madogo angalau saba(07) kwa ajili ya mazoezi, Begi la kubeba madaftari (mikoba hairuhusiwi),graph paper kwa wanafunzi wa **CBG** na Kamusi(Oxford Advanced Learner’s Dictionary, 9$^{th}$ edition) kwa wanafunzi wa **HKL.**
- **Cheti cha matokeo ya kidato cha nne (Result Slip)**

### B. MAHITAJI MENGINE MUHIMU

- Ream 1 ya karatasi nyeupe A4 kwa mwaka.
- Ream 1 Ruled Paper (yenye mistari) kwa mwaka
- Vitabu vya masomo ya tahasusi husika Kwa matumizi yake binafsi.(orodha ya vitabu husika imeambatanishwa) (kiambatanisho na. 5)
- ***Dissecting kit na tray kwa wanafunzi wa Biolojia (Mwanafunzi anayesoma anapaswa kununua) itakaguliwa wakati akifika shuleni.***
- Shuka mbili rangi ya bluu bahari (light blue) iliyokolea, Blanketi moja, mto na foronya
- Godoro la futi mbili na nusu
- Sanduku la bati 1(Tranker)

- Taulo,kanga/kitenge jozi moja, nguo za ndani za kutosha na vifaa muhimu vinavyomhusu msichana (Ped) Taulo za kike
- Sabuni za kufulia na kuogea za kutosha, mafuta ya kujipaka**(marashi na mafuta yenye harufu kali mengine yanayobadilisha rangi ya ngozi hayaruhusiwi)**
- Vyombo vya chakula: Bakuli la cello la plastiki lenye mfuniko la plastiki, kikombe cha plastiki, kijiko na kandambili *(Pia vinauzwa duka la shule kwa wale wasiokuja navyo)*
- Ndoo mbili ndogo zenye mifuniko.
- **Vifaa vya usafi**

**CBG –**Squizer 1, Sabuni ya maji ya chooni lita 5**,** Fyekeo 1.
**HKL -** Hard broom 1, Sabuni ya maji ya chooni lita 5, Fyekeo 1.

## 3 MICHANGO YA SHULE

### a) Michango inayotakiwa kulipwa na kila mwanafunzi ni:

**Shule za Bweni**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

Angalizo michango yote ya shule iliyoainishwa hapo juu ilipwe kwenye akaunti **No 40401100033 NMB** yenye jina la **HOROMBO SEC RECCURENT ACCOUNT** na Mwanafunzi aje na Bank pay slip siku ya kuripoti.Aidha mchango wa Uendeshaji unaweza kulipwa kwa awamu mbili

**NB:** Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa na bima ya afya. kwa wanafunzi wote wenye bima ya afya ya **NHIF** au nyingine yoyote waje nazo shuleni. Shule haitahusika na gharama za matibabu ya mwanafunzi.

.

## 4. FOMU MBALIMBALI KWA MZAZI NA MWANAFUNZI ZA KUJAZA:

Fomu mbalimbali za kujazwa na mzazi/mlezi pamoja na mwanafunzi zimeambatanishwa.

**4.1 Sheria, kanuni na taratibu za shule zilizoambatanishwa**, ***mwanao azisome vizuri na kuzielewa na awe tayari kufuata maelekezo na taratibu nyingine za shule.*** Mwisho tunamtakia mwanao safari njema ya kuja hapa Shule ya Sekondari Horombo.

***4.2 Ni muhimu sana mwanao kupima afya na apewe risiti ya EFD mashine na iletewe shuleni siku ya kuripoti.***

**Asante na karibu sana katika shule yetu.**

**…………...**

**ELINE S. LEMA**
**MKUU WA SHULE**

**NB:** ***Mzazi/mlezi tunaomba uthibitishe mwanao kujiunga na shule yetu mara tu upatapo nafasi ya uchaguzi wa serikali wakati ukiendelea na maandalizi mengine kwa namba 0784347795 (Mkuu wa shule) au 0782921188 (Makamu mkuu wa shule). Changamoto yoyote itakayojitokeza wasiliana na uongozi wa shule.***

**(KIAMBATANISHO Na. 1)**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA ROMBO**
**SHULE YA SEKONDARI HOROMBO**

**SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995.

Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na **Ofisi ya Rais – TAMISEMI** yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

## Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake wawapo shuleni bila idhini ya mwanafunzi husika.
xii. Mwanafunzi hapaswi kuja na simu/line shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;
xiii. Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;
xiv. Mwanafunzi hataruhusiwa kurudi nyumbani kipindi chote cha masomo bila kibali maalum toka kwa uongozi wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).

**Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo; kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wetu ndani nan je ya shule.
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele .
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na biashara na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, usagaji, ushoga na ulawiti.
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kwenda kwenye maeneo yasiyoruhusiwa bila kibali maalum
xiv. Kumiliki, kukutwa na laini au kutumia simu ya mkononi isiyoruhusiwa katika mazingira ya shule. Simu zinazotumiwa ni zile zilizoelekezwa na uongozi wa shule tu.
xv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvii. Uharibifu wa mali ya umma nay a watu wengine kwa makusudi.
xviii. Kukataa adhabu iliyotolewa na mwalimu
xix. Kukataa kufanya mazoezi na mitihani

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule: 0784347795 /0652190906**
- **Makamu Mkuu wa Shule: 0782921188/0756455756.**
- **Mwandamizi Taaluma: 0765116541/0679116541/0717511084**
- **Mwandamizi Malezi: 0752869009/0762979428**

**(KIAMBATANISHO NO 2)**

**MKATABA NA KAULI YA KUKUBALI KUTII SHERIA, KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE**

Mimi… ........................................................................................... (*Jina la mwanafunzi*)

Ninakiri kuwa nimesoma na kuzielewa vizuri sheria, kanuni na taratibu za shule kama zilivyoainishwa katika vipengele vyote, na kuwa mara nikiukapo sheria hizo hatua za kinidhamu zichukuliwe kama zilivyoainishwa dhidi yangu.

JINA LA MWANAFUNZI……………………………………………..

SAHIHI YA MWANAFUNZI……………………………………………..

TAREHE………………………………………………………………….

Mimi ……………………………………………………….(*Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi*) wa mwanafunzi……………..…………...(*Jina la mwanafunzi*) wa kidato cha……………… tahasusi(*comb.)* ya………………..

Nakiri kupokea, kusoma na kuzielewa taratibu zote zilizo kwenye maagizo ya kujiunga na shule ya sekondari ya Horombo. Iwapo mwanangu atakiuka taratibu hizo nitakuwa tayari kukubali hatua zitakazochukuliwa dhidi yake na shule. Nitakamilisha mahitaji yote ya shule kwa wakati.

JINA LA MZAZI/MLEZI ………………………………

Namba za simu…………………………………………………

SAHIHI YA MZAZI/MLEZI…………….………………………

TAREHE……………………………………...

Namba ya simu ya ndugu/Jamaa wa karibu………………………………….

**(KIAMBATANISHO NO 3)**

**PRESIDENT'S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT HOROMBO SECONDARY SCHOOL**

## MEDICAL EXAMINATION FORM

To be completed by a medical Officer in a Government hospital.

STUDENT'S FULL NAME: …………………………………………………………

AGE: …………………………………………………...

1. Blood count (Red and White): ……………………………………………
2. Stool Examination: ……………………………………………………
3. Urine Examination: ………………………………………………………………….
4. Eye test: ………………………………………………………………
5. Ear test: …………………………………………
6. Speech test: ………………………………………………………………………
7. T.B test: ……………………………………………………………………………
8. STD test: ……………………………………………………………………………
9. Spleen: ……………………………………………………………………………
10. Abdomen: ……………………………………………………………………………
11. Additional information from any Physical, Mental, Hereditary diseases or disabilities:

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

*Treatment after Examination*:

………………………………………………………………………………………

MEDICAL CERTIFICATE

*I certify that the above-mentioned student has been thoroughly examined by me and found fit/unfit to pursue further education.*

*SIGNATURE*: ……………………………………………………………

*DESIGNATION/STAMP*……………………………………

*DATE*: ……………………………………………………………

*STATION*: ………………………………………………………

**(KIAMBATANISHO NO 4)**

**SHULE YA SEKONDARI HOROMBO,**
**S.L.P 145**
**MKUU ROMBO.**

**TAREHE………………**

## MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI

**JAZA FOMU HII KWA UKWELI**

**TAARIFA ZA MWANAFUNZI**

**IJAZWE KWENYE JEDWALI HILI**

| **MAJINA** | **La kwanza** | **La kati** | **La mwisho** | **UMRI** | **TAREHE YA KUZALIWA** |
|---|---|---|---|---|---|
| Majina ya shuleni | | | | | _ |
| Majina ya nyumbani | | | | | |

2. **NYUMBANI:**

Kijiji/Mtaa……………Kata…………………Tarafa……………….Wilaya…………Mkoa…………………

3. Anwani ya nyumbani………………… Simu …………………………

4. Kukiwa na matatizo taarifa ipelekwe kwa nani?

JINA: ………………………………………………………..…..

Uhusiano na wewe? ..........................................................................................

Anafanya kazi gani na wapi…………………………………………………………

5. **Wazazi na Ndugu**:

Majiana ya (i) Baba ……………………………………………………
(ii) Mama……………………………………………………..

Baba yuko hai? .................................Mama yuko hai? ................................

6. Dini yako …………………………………madhehebu ……………………………….

**TAARIFA ZA WATEGEMEZI**

a) Unaishi na nani na wapi? ........................................... simu yake………………………

b) Nani anayekupa mahitaji ya shule :……………………simu yake………………………
SAHIHI:…………………………………..

c) Wakati wa likizo utaenda wapi… …………….uhusiano…………………anaishi wapi…………….namba ya simu……………………………………

d) Majina ya watu 4 watakaohusika kuwasiliana na uongozi wa shule endapo utahitajika kwa suala lolote lile.

| | JINA | ANWANI | SIMU | UHUSIANAO | MAHALI ANAPOISHI |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | | | | | |
| 2 | | | | | |
| 3 | | | | | |
| 4 | | | | | |
| | | | | | |

**PICHA ZA WATU WANAOHUSIKA KUWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE**
**(Bandika picha za passport size za hivi karibuni)**

**NB:** Kila mwanafunzi ahakikishe kuwa amebandika picha za watu atakaokuwa anawasiliana nao akiwa shuleni.
Picha hizi zitakaguliwa wakati mwanafunzi atakaporipoti shuleni.

**(KIAMBATANISHO NO 5)**

Vitabu vya masomo ya tahasusi husika kwa matumizi binafsi ya mwanafunzi. Mwanafunzi achague kulingana na tahasusi yake.

**1. Chemistry**

-Raymond chang

-Chand II & II

-Rymsden 6th addition

-Advanced chemistry Peter Alctin

-Mzumbe book Project-Organin part I

-Inorganic part I & II

-Physical Chemistry

2. **Biology**

-Understanding biology

-Biological science

-Function approach

-Chand

**3. Geography**

-Principles of physical Geography by Monkhouse J.

-Integrated Approach to Geography by David Waugh

-Regional Geography by D.T. Msabila

-Practical Geography for Africa by Pritchard John

-Physical Geography – Bunnet

-Research Methodology by Kothan

.

**4. General Studies**

-General studies for Advanced Certificate form five and Six by Richard Mbalase.

-Understanding Advanced General Studies (form 5 and 6) by Johanes Bigirwamungu.

**5. BAM**

-Basic applied mathematics by Wakamoga Masinde

-Basic Applied Mathematics by gdy publication.

**6. KISWAHILI**

-Massamba D.P () Sarufi maumbo ya Kiswahili sanifu TUKI, Dar es salaam.

-Massamba D.P na wenzake () Sarufi miundo ya kiswahili sanifu TUKI, Dar es salaam.

**RIWAYA**

(1) Shafi Adam (1999) **Vuta ni kuvute** Mkuki na Nyota publishers LTD, Dar es Salaam.
(2) Msokile . Mbunda (2007) **Usiku utakapokwisha** Macmillan Aidan LTS Dar es Salaam.
(3) Tuwa Hussein (2007) **Mfadhili** Macmillan Aidan LTD Dar es Salaam.
(4) Robert . S. ( ) **Kufikirika**. Oxford University Press Nairobi.

**TAMTHILIYA**

(5) Hussein Ebrahim (1988) **Kwenye Ukingo wa Thim** Oxford University Press

(6) Mohamed .S. (1990) **Kivuli Kinaishi** Oxford University Press Nairobi.

(7) Muhando P. (2007) **Nguzo Mama** Macmillan Aidan Ltd Dar es Salaam.

(8) Mbogo Emmanuel ( 2007) **Morani**. Macmillan Aidan Ltd Dar es Salaam.

**USHAIRI**

(9) Mvungi T. (1985) **Chungu Tamu** T.P.H Dar es salaam

(10) Khatibu S. (2007) **Fungate ya Uhuru** Macmillan Aidan LTD Dar es Salaam

(11) Haji Gora ( 2001) **Kimbunga** TUKI Dar es Salaam.

(12) Robert S. ( ) **Mapenzi Bora** Mkuki na Nyota Publishers Dar es Salaam.

**7. ENGLISH**

(1) Oxford Advanced Learners Dictionary
(2) Advanced Level English: A Practical Aproach.Nicholaus Asheli,Good Book Publishers.
(3) Literature for advanced level:Godfrey Ruta Bukagile.Nyambari Nyangwine Publishers .
(4) English for A level—Oxford.
(5) Advanced level English language & structure and stylistic : Nicholaus Asheli
(6) English language paper 2 – Nicholaus Asheli

**8. HISTORY**

(1) Advanced Level History paper one N. A. paper two. Kato Abubakar
(2) Essentials in Advanced History.
(3) Major issues in African History Advanced level - Dar –es –salaam University Press - 1996